# Ulega afanya ziara Lindi, atoa injini ya boti na mwani

Lindi
NA SOPHIA NYALUSI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameaza ziara ya kutembelea wilaya tano za Mkoa wa Lindi, lengo likiwa kusikiliza kero za wakulima, wafugaji na wavuvi.

Akizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi Ulega alisema amebaini kuwepo kwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya ya Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa, lakini kuna baadhi ya mapungufu.

Ulega alisema ziara yake imebaini mapungufu kwa baadhi ya wasimamizi wa shera katika kutoa haki kwa usawa baina ya makundi na wananchi wengi imesababisha baadhi yao kutokuwa na imani.

Ulega alisema wizara imetenga fedha kwa ajili ya mradi wa mabwawa katika Wilaya ya Liwale na Nachingwea zaidi ya sh. milioni 480 na majosho nane kwa Wilaya ya Liwale (3) Nachingwea (1) Ruangwa (2) Kilwa (2).

Hata hivyo, Ulega alisema wizara imetoa fedha na kama kutakuwa na tatizo lolote iko tayari kutoa ushirikiano wa dhati kuhakikisha malengo ya mkoa yanafikiwa katika sekta ya mifugo na uvuvi.

"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ipo tayari kuhakikisha inatatua migogoro ya wafugaji nchini ili kila mwananchi awe na haki ya kulima, kufuga na kuvua samaki," alisema Ulega.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, alimpongeza ze Naibu Waziri Ulega kufanya ziara katika mkoa huo na kuweza kutatua migogoro iliyopo katika wilaya.

Telack alisema walikuwa na migogoro mingi ya ardhi, lakini kwenda kwa Ulega kumepunguza migogoro hiyo hivyo alishukuru ushirikiano ulioonyeshwa na kiongozi huyo na kuomba uendelee.

Katika hatua nyingine, Ulega alikabidhi injini ya boti yenye ukubwa wa HP 40 na thamani ya sh. milioni 11 na kamba za kuzalisha mwani 1,216 yenye gharama ya sh. milioni nane.

Akizungumza katika kikao na wananchi wa Jimbo la Mchinga, Ulega alisema serikali kwa kushirikiana na washiriki wa maendeleo inaendelea kusimamia na kuendeleza shughuli za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji nchini.

Ulega alisema katika kukabidhi mwani kuna vikundi vitatu na kila kikundi kitapewa kamba 405 ili kuendeleza kinamama wasikae bila shughuli na juhudi zote zimepelekwa na Mbunge wao Salma Kikwete.

Ulega alisema ahadi ya Serikali ya Awamu ya Sita imetimizwa, hivyo aliwaomba wavuvi waendele kufanya kazi kwa juhudi zote na serikali ipo kwa ajili yao wananchi wa Mchinga na mbunge wao anaendelea kuwasemea katika kuhakikisha wanawake wanafanya kazi nzuri za ujasiriamali.


"Naagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wote katika wilaya zote za Mkoa wa Lindi, vikundi hivi vya mwani viwezeshwe kuwa na ushirika ili kinamama waendelee kukuza uchumi wao," alisema Ulega.

Alifafanua kuwa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia imeweza kutoa fedha zaidi ya sh. milioni 11 kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mchinga katika kuhakikisha boti zinatumika vizuri na wavuvi wanafanya shughuli zao kwa urahisi.

Ulega aliwaomba kinamama wa Jimbo la Mchinga kuunda vikundi kwa ajili ya kupeleka mradi wa kuku ili kuwapa hamasa ya kuendelea kufanya ujasiriamali kikamilifu.

Kwa upande wake, Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete, alimpongeza Naibu Waziri Ulega kwa kupeleka injini ya boti na mwani kwa ajili ya wananchi wa jimbo hilo.

"Furaha ya Leo imezidi kifani kwa wananchi, serikali imetoa fedha kubwa katika jimbo la Mchinga naomba nimpongeze Rais Samia kwa kutenga fedha kwa ajili ya wananchi," alisema Salma.




NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia) akimkabidhi injini ya boti yenye thamani ya sh. milioni 11 kwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga (CCM), Salma Kikwete pamoja na Kikundi cha Wavuvi wa Mchinga mkoani Lindi, jana. (Picha na Sophia Nyalusi).

# Walimu wacharazwa viboko na

Scanned with CamScanner

wa wananchi waliotapeliwa kwa kuuziwa sehemu ya eneo hilo, alisema alitoa sh. milioni 1.5 akauziwa kipande cha ukubwa wa mita 15 kwa 20 anasikitikia hasara aliyoipata.

CCM hawezi kukubaliana na upuuzi huo.

Awali, akitoa malalamiko kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Nianjema, Mwenyekiti

DUWASA wamefanya miundombinu rafiki ikiwemo kufanya ukarabati wa mifereji ya kusafirishia maji taka na utanuzi wa mabwawa hayo ili kurahisisha uhifadhi wa maji taka katika maeneo mbalimbali ya mji.

"Kama Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji tunawapongeza DUWASA kwa juhudi na hatua wanazo zifanya kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri,"alisema.

Kilima aliongeza kuwa: "Tumejaribu kutembelea miundombinu ya mabwawa yanayotumika kuhifadhia maji hayo tumeona yana ridhisha na ya kiwango cha kimataifa."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema kwa sasa mamlaka hiyo inafanya ukarabati wa miundombinu ya kusafirishia maji taka ikiwemo kuzibua na kukarabati mifereji ya kupitisha majitaka katika maeneo ya Area C na D ambayo mifumo yake ilikuwa ya muda mrefu.

Aidha, mhandisi Joseph alisisitiza kuwa kwa sasa mamlaka hiyo imeweka mifumo imara ya kusafirisha majitaka kutoka maeneo ya mjini hadi kufika katika mabwawa maalumu ya kuhifadhia.

"EWURA wamekuja kutembelea kuona jinsi gani tulivyo jipanga kuhakikisha huduma ya majitaka inakuwa ya kuridhisha jijini Dodoma na tunawahakikishia wananchi kuwa huduma hii itakuwa ya kuridhisha, "alisema mhandisi Joseph.

Naye, mkazi wa Chinangali jijini Dodoma, John Tamim, alisema kwa kipindi kilichopita mifumo hiyo ya maji taka katika maeneo yao ilikuwa ni changamoto kidogo, hivyo kutokana na juhudi za DUWASA kukarabati hatimaye kwa sasa wanapata huduma ya kuridhisha na bora kwa mahitaji yao.



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza katika mkutano na wananchi wa Kitongoji cha Mwanduhubantu, Kijiji cha Mpeta, Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma, wakati akikabidhi ekari 6,000 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa wananchi 5,900 waliovamia eneo la ranchi ya Malai wilayani humo na kuongezwa kuwa sehemu ya makazi ya wananchi hao. (Picha na Fadhili Abdallah)

# Maziwa mengi nchini uharibika - Msajili

Morogoro
**NA LATIFA GANZEL**

LICHA ya Tanzania kuzalisha takribani lita bilioni 3.4 za maziwa, bado ni asilimia tatu tu huingia kwenye mfumo rasmi wa uuzaji maziwa na mengine kupotea.

Hivyo wafugaji na wasindikaji wa maziwa wamehimizwa kuzingatia utunzaji, uhufadhi na usafi wakati wa uandaaji ili kulinda afya za walaji na kuongeza soko.

Hayo yalibainishwa juzi na Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. George Msalya, wakati wa makabidhiano ya vifaa vitakavyotumika katika mnyororo wa kukusanya, kuhifadhi na kusambaza maziwa kwa vikundi vya wafugaji wanawake wilayani za Mvomero na Kilosa mkoani Morogoro, vifaa vilivyotolewa na Shirika la Heifer International.

"Maziwa ni uchumi, ni biashara ni lazima tufanye kazi kwa weledi ili maziwa yaweze kutunufaisha,"alisema.

Dk. Msalya alisema maziwa ni bidhaa ambayo ni rahisi kuharibika kama hayakuhifadhiwa vizuri na kwa usafi.

Alisema ni wakati sasa wafugaji na wasindikaji wa maziwa kubadilika na kuhakikisha maziwa hayo yanahifadhiwa kwa usafi ili yawe salama hadi yanampomfikia mlaji.

" Wengi wanatembeza maziwa yaliyohifadhiwa katika chupa za maji ya kunywa zilizotumika, hali hiyo slo salama kabisa,"alisema

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash, aliwataka wanawake waliopata fursa ya kupewa vifaa hivyo kuitumia vyema ili kutoa nafasi kwa wengine kupata fursa hizo.

"Miaka ya zamani wanawake ilizoeleka ni watu wa kukaa nyumbani tu bila kujishughulisha na kipato, lakini sasa wanawake wako mbele katika shughuli za uchumi,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Wafugaji Mkoa wa Morogoro, Shambakubwa Longido, alisema wanaume jamii ya Wamasai kwa sasa wanafurahishwa na wanawake zao kwa kusaidia kuboresha pato la familia badala ya kumtegemea mwanaume kama ilivyokuwa awali.

Katibu wa kikundi cha kina mama Newangai cha Wami Dakawa ambacho ni miongoni mwa wanufaika, Eva Ikoneti, alisema kwa sasa wanafanikiwa kukusanya maziwa mengi na bila kuharibika kutokana na vifaa walivyopewa na Shirika la Heifer International.

Mkurugenzi wa Heifer International, Mark Tsoxo, alisema mradi huo umeweza kuwafikia wafugaji zaidi ya 1,000 ikiwa ni zaidi ya asilimia 100 ya malengo.

Aidha, alisema katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa maziwa, mradi umeweza kutoa vifaa wezeshi vya kuhifadhia na kupooza maziwa ambayo ni matanki mawili yenye uwezo wa lita 10,000, jenereta na kuboresha vituo vya ukusanyaji maziwa shughuli zikizogharimu sh. milioni 254.9.

Scanned with CamScanner

# Viongozi wa vijiji wanavyochochea migogoro ya wakulima na wafugaji



**NA MWANDISHI WETU**

WILAYA ya Kilosa mkoani Morogoro imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya migogoro ya ardhi kwa muda mrefu, licha ya serikali imekuwa ikifanya jitihada za kumaliza tatizo hilo.

Kilosa ambayo ni maarufu kwa kilimo cha mazao ya kibiashara na shughuli za ufugaji zinazofanywa na jamii ya Wasukuma wa Wamasai, migogoro ya ardhi imekuwa ikijirudia mara kwa mara na kuhatarisha amani.

Kwa mujibu wa baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kilosa, migogoro hiyo imekuwa ikisababishwa na baadhi ya viongozi wa vijiji kutokuwa waadilifu ambao wamekuwa wakitanguliza maslahi yao mbele kwa kijihusisha na rushwa ili kuwakaribisha wafugaji kuingia katika maeneo ya wakulima.

Mkazi wa Kijiji cha Kivungu, Kata ya Kilangali, wilayani Kilosa, Frank John, anadai baadhi ya wenyeviti wa vijiji wamekuwa wakipokea kitu kidogo kutoka kwa wafugaji ili kuruhusu mifugo kuingia wilayani humo.

"Tatizo hilo linasababishwa na viongozi wetu wa ngazi ya chini, tumekuwa tukiwaonya kuhusu suala hili, lakini hawataki kusikia ushauri wetu, hivyo mifugo imekuwa ikiingia wilayani hapa kila mara,"anasema.

John anaeleza kuwa wafugaji wanapoingiza mifugo kwa wingi, wanakosa maeneo ya malisho, hivyo kulazimika kuingiza mifugo shambani na kusababisha uvunjifu wa amani maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Mbali na mgogoro wa wafugaji wa wakulima, kwa sasa kumeibuka mgogoro kati ya wafugaji wa jamii ya kimasai na kisukuma, hali inayosababisha viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Mgogoro wa ardhi umezidi kushamili hapa Kilosa kwani awali ulikuwa ni wa wakulima na wafugaji lakini kwa sasa wafugaji wa jamii ya wasukuma na wamasai nao hawaelewani, wamekuwa wakigombana kila siku kukicha,"anasema John.

Naye, Sabato Kombe, anasema mbali na viongozi wa serikali ya vijiji na kata kutokuwa waledi wa kutetea maslahi ya wananchi, baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo kukosa uelewa wa masuala ya haki ardhi ni miongoni na sababu ya migogoro hiyo.

Kilosa ambayo ni maarufu kwa kilimo cha mazao ya kibiashara na shughuli za ufugaji zinazofanywa na jamii ya Wasukuma wa Wamasai, migogoro ya ardhi imekuwa ikijirudia mara kwa mara na kuhatarisha amani.

Kombe anasema ni voingozi hasa wa vijiji wamekuwa wakipokea rushwa kutoka kwa wafugaji wanaohamia na kusababisha kuwepo kwa uhaba wa malisho katika wilaya hiyo.

"Kilosa imeshamili kwa migogoro ya ardhi, ni kweli wafugaji wamekuwa chanzo cha migogoro hii, lakini wananchi wengi hawana elimu ya haki ardhi hivyo kukosa uelewa kuhusu mpango bora wa matumizi ya ardhi hapa Kilosa," anasema Kombe.

Anasema ili kukabiliana na changamoto hiyo, viongozi wa vijiji vyote vilivyoshamili kwa migogoro waundiwe tume ya uchunguzi na hatua zichukuliwe kwa watakaobainika.

Mfugaji wa jamii ya kimasai, Ruben Oraita, ambaye hivi karibuni alishambiliwa kwa mapanga maeneo mbalimbali na wafugaji wa kisukuma hadi kulazwa katika hospitali ya Dumila, anasema bado kunahitajika nguvu kumaliza migogoro hiyo.

Anasimulia kuwa siku ya tukio akiwa akilisha mifugo yake alivamiwa na kundi la wasukuma kisha kumshambulia kwa mapanga hadi kupoteza fahamu.

Mfugaji huyo anaiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi waishi kwa kueshimiana kwani ili wilaya hiyo iendelee kuwa na amani.

Mkazi wa Kilosa Mjini, Rose Benson, anasema chanzo cha migogoro hiyo ni baadhi ya wafugaji kuwahonga fedha viongozi kuruhusu mifugo kuingia kwa wingi maeneo mbalimbali ya vijijini.

"Ukienda kulalamika kwa mamlaka zinazohusika kuhusu uonevu uliofanywa na wahalifu hasa wafugaji, baadhi ya viongozi hushirikiana nao kuwapa taarifa kwa kile kinachoendelea na kusababisha mlalamikaji kukosa haki,"anasema Rose.

Anasema kuwa kutokana na hali hiyo baadhi ya wananchi hasa wakulima wanajichukulia sheria mkononi jambo ambalo limekuwa likichafua taswira ya wilaya hiyo ambapo ameomba viongozi wote wa namna hiyo waondolewe.

Rose ameiomba serikali na wadau wengine wa kisheria kuendelea kutoa elimu kwa jamii kusaidia kupunguza migogoro hiyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilangali, Lesheine Mlonga, anakili kuwepo kwa baadhi ya wenyeviti ambao sio waadilifu wanaosababisha migogoro ya ardhi.

KAULI YA SERIKALI

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, amelaani vitendo vya uvunjifu wa amani vinavyoendela katika wilaya hiyo.

Amesema tayari viongozi wanaodaiwa kupokea rushwa wameshaanza kukamatwa.

"Serikali haiwezi kulifumbia macho suala hilo, wote wanaohusika kupokea rushwa kutoka kwa wafugaji kuruhusu mifugo yao kuingia wilayani hapa kwa njia za panya, tutawakamata na kuwachukulia hatua kali,"anasema Mwanga.

Amewapongeza wadau wa haki za ardhi kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ardhi ambapo aliwataka wananchi kutumia fursa hiyo kuepuka changamoto ya migogoro itokanayo na ardhi katika wilaya hiyo.

Ofisa Programu Mwandamizi wa Hakiardhi, Joseph Chiombola, anaeleza katika kuondoa changamoto hiyo, wakulima na wafugaji wanatakiwa kujiepusha na uharibifu wa mazingira uliopo hivi sasa.

Anasema wananchi wamekuwa wakijihusisha na uharibifu wa mazingira bila kujali athari zake hali inayochangia kuwepo kwa mabadiliko ya tabia nchi na kusababisa changamoto kwa wakulima na wafugaji.

Anaeleza kuwa elimu kwa wafugaji na wakulima kuhusu utunzaji mazingira itasaidia jamii kutunza mazingira ili kuepuka athari zake ambazo ni magonjwa, uhaba wa chakula pamoja na migogoro ya ardhi.

Ofisa huyo anasema mbali na mabadiliko ya tabia nchi, jamii za wakulima na wafugaji bado hawana uelewa mzuri kuhusu umiliki wa ardhi.

Chiombola anasema taasisi ya hakiardhi kwa kutambua umuhimu huo imekuwa ukitoa elimu kwa jamii kuhusu umiliki wa ardhi wa katika jamii zote.

Anasema ardhi ya Tanzania imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ardhi ya kijiji, hifadhi na jumla.

Anafafanua kuwa ardhi ya kijiji ni ile iliyo ndani ya mipaka ya kijiji, ardhi ya hifadhi ni ile iliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalum kama hifadhi za taifa za wanayapori, milima, misitu na barabara huku ardhi ya ni ile iliyobaki baada ya kuondoa kijiji na hifadhi kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina ilibainika kuwa baadhi ya wafugaji hawana uelewa wa haki ya kumiliki ardhi kitendo ambacho kimekuwa kikichochea migogoro ya ardhi maeneo mbalimbali katika jamii zao," anasema Chiombola.



Scanned with CamScanner

walivyokutwa na mpigapicha wetu Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, jana. (Picha na Benedict Mwasapi).

UHURU UK 19

# Bil. 23.3/- kujenga ofisi za Wizara ya Mifugo

**Dodoma**
**NA FRED ALFRED**

SERIKALI imetoa sh. bilioni 23.3 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa tano za ofisi za Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Mifugo Dk. Rashid Tamatama (Uvuvi) aliyasema hayo juzi baada ya kusaini mkataba wa kuanza kwa ujenzi huo.

Alisema jengo hilo litajengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika ya kipindi cha miezi 24 huku ujenzi ukitarajiwa kuanza Oktoba 14, mwaka huu ambapo awamu ya kwanza serikali imetoa sh. bilioni 4.6.

"Katika mchakato unaoendelea wa ujenzi wa majengo ya serikali hapa Mtumba, Wizara ya Uvuvi na Mifugo tunakabidhi eneo la ujenzi wa jengo la wizara ambapo tunatarajia kuanza na wingi "A" na ujenzi wake utatekelezwa kwa awamu mbili kwa muda wa miezi 24," alisema.

Alifafanua kuwa katika awamu ya kwanza ambayo wataanza hivi karibuni fedha zilizotengwa kutekeleza mradi huo ni sh. bilioni 4.6 na inatarajiwa hadi jengo hilo kukamilika miaka miwili ijayo gharama ya ujenzi itakuwa imefikia sh.bilioni 23.3 ambapo jengo litakuwa na ghorofa tano na ghorofa ya chini.

Dk. Tamatama aliwataka NHC kuhakikisha wanamaliza ujenzi kwa wakati huku wakizingatia ubora ili thamani ya fedha ionekane.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo, Amos Zefania, alisema ujenzi wa ofisi hiyo utaleta manufaa kwa watumishi kwa sababu utapunguza gharama za uendeshaji.

Alisema kwa sasa wizara imegawanyika kwani ofisi zake zipo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) jengo la NBC na Mtumba hivyo kufanya watumishi kuhangaika.

"Kukamilika kwa jengo la wizara kutapunguza gharama za uendeshaji, na kuongeza ufanisi kwasababu mazingira ya kazi ya watumishi yataboreka,"alisema.

Aliongeza kuwa:" Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha ili tujenge na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwasababu ndio msingi wa kuongeza ufanisi na tija katika kazi."

Mkurugenzi Mtendaji wa NHC, Maulid Banyani, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwaamini na kuwapa miradi mikubwa na kuuhakikishia uongozi wa wizara kuwa ujenzi wa jengo hilo utakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora.

"Ujenzi huu utazingatia thamani ya fedha kwasababu ni muhimu sisi kama wafanyabaishara tufanye kazi vizuri ili tutengeneze mazingira ya kupata kazi nyengine," alisema.


# Watanzania watakiwa kuacha visingizio chanjo

**Dodoma**

zinazotolewa maeneo ya pembezoni mwa

wananchi ili wao wenyewe ndio wachague

THE GUARDIAN Page 3.



Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega addresses herders and farmers at Nangurugai in Ruangwa District yesterday at a meeting called to seek an end to various disputes in the village. Photo: Mbaraka Kambona

Kiyegeya Bridge follows the collapse of the old bridge 18 months ago forcing the government to construct a temporary bridge nearby that has been in use ever since.

THE GUARDIAN Page 4



# Hygienic milk handling and processing vital for livestock keepers, says TDB registrar

**By Guardian Correspondent, Mvomero**

LIVESTOCK keepers and milk processors in the country have been called to adhere to proper storage and cleanliness for their raw materials to protect the health of their consumers as well as to add value to the products.

The remarks were made here yesterday by Tanzania Dairy Board (TDB) registrar Dr. George Msalya during the handing over of equipment to be used in the whole chain regarding collection, storage and distribution of milk to women livestock keepers' groups in Mvomero and Kilosa districts in Morogoro Region provided by Heifer International.

Msalya said even though Tanzania producing 3 billion litres of milk, only three per cent enters formal milk sales, the other is lost through unhygienic unofficial sales including in plastic bottles, while the rest gets bad through improper storage.

He said milk is economy, business and food with lots of vitamins, proteins, fats minerals and other nutrients, all of which were important in one's diet, hence processors and distributers must store the commodity properly.

Mvomero District Commissioner, Halima Okash called on women who received the equipment and training to utilize well the opportunities so as to make other women to be trusted for similar assistance.

He said for a long time it was discovered that women were people staying in homes without any activities for their economic wellbeing, but now they are at the forefront in productive economic activities.

Morogoro Region Livestock Keepers Chairman, Shambakubwa Longido said men in the Maasai communities were now happy for their women engaging in income generation for their families.

For his part, the Secretary of Newengai Women Group from Wami-Dakawa in Mvomero District, Eva Ikoneti who also is beneficiaries of the hand out of the dairy equipment said as for now they were collecting much more milk using the equipment provided by Heifer International, including motorcycles, a generator and a freezer.

For his part, Heifer International Director, Mark Tsoxo said the project has reached more than 1,000 livestock keepers, equivalent to one per cent of their set target.

He said the equipment provided included two 10,000-litre storage tanks for milk, a 20KVA power generator all valued at 254.9m/-.

**He said milk is economy, business and food with lots of vitamins, proteins, fats minerals and other nutrients, all of which were important in one's diet, hence processors and distributers must store the commodity properly**

Scanned with CamScanner

uk 11 uk 10, uk 5, 19

## Viongozi vijijini wanavyochochea migogoro ya wakulima na wafugaji

Uk. 14

# UHURU Vijijini

ISSN 0876 - 3896 Na. 24109 Ijumaa
Septemba 24, 2021 Tanzania sh. 1,000



## Ulega afanya ziara Lindi, atoa injini ya boti na mwani

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameaza ziara ya kutembelea wilaya tano za Mkoa wa Lindi, lengo likiwa kusikiliza kero za wakulima,

Uk. 5

Walimu...

# Rais Samia atikisa UN

- Hotuba yake ya kwanza yagusa wajumbe ukumbini
- Aangazia mambo muhimu ikiwemo Corona, usawa wa kijinsia na mabadiliko ya tabianchi

Uk. 4



## Dk. Mpango awatak[a] mabalozi kusaka teknolojia na mita[...]



## IGP Sir[...] amsha[...] msaii[...]

Scanned with CamScanner